LATRA
IMETHIBITISHWA ISO 9001

# SERA YA UBORA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), ilianzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 kwa lengo la kudhibiti usafiri ardhini kibiashara ikiwemo usafiri wa barabara, reli na waya.

Tumejizatiti kudhibiti huduma za usafiri ardhini kibiashara kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (QMS) ISO 9001 katika michakato yote inayohitajika ndani ya Mamlaka.

Sera yetu ya ubora ni kuendelea kutoa huduma zinazokidhi au kuzidi mahitaji na matarajio ya wateja wetu, wakiwemo watoa huduma zinazodhibitiwa, watumiaji huduma zinazodhibitiwa na wadau wengine.

Tunaendeleza ubora huu kupitia programu zinazomuwezesha kila mtumishi wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa usahihi kila wakati, kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusika, pamoja na viwango vya udhibiti, na malengo na malengo ya ubora ya QMS ISO 9001.

***Pamoja kwa Usafiri Bora***

CPA Habibu J. S. Suluo
MKURUGENZI MKUU
1 Julai 2024